

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 11 mwezi 03 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi cha VETA ARUSHA S.L.P. 509, OLJORO, ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802 DODOMA (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwaiiri") kwa upande mmoja;

NA

ISRAEL ISMAEL KAAYA S.L.P. \_\_\_\_\_, ARUSHA  
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Local Fundi") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri anaendelea na ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya LONGIDO;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya LONGIDO;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya kutengeneza makaro ya kufulia fengo la hosteli ya wavulana na fengo la wasichana;

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundi nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 500,000, Fundi atafanya kazi ya

kutengeneza makaro ya kufulia fengo la hosteli ya wavulana na fengo la wasichana

kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

## 2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

## 3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 50 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 45% ya Gharama ya Ufundi/Kazi;
- (c) Baada ya kukamilika kwa muda wa matazamio: 5% ya Gharama ya Ufundi/Kazi.

## 4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

- (a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe 21 mwezi 03 2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.
- (b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 30 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.
- (c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

## 5. WAJIBU WA FUNDI

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

- (a) Kujenga Maliko na kukamilisha ujenzi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaavya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;
- (b) Kumpatia Mwajiri ratiba ya kazi (*work programme*) ndani ya siku 7 tangu tarehe ya kusaini Mkataba huu ili kupata kibali cha Mwajiri.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI CHA ARUSHA.

Jina: ISLAEEL ISMAEL KAAYA Saini: *Isaac*

Wadhifa: FUNDI: UASHI Tarehe: 11-03-2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: AMANI KOFFIE LONY Saini: *Amani*

Wadhifa: UASHI Tarehe: 11-03-2022

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: GEORGE MOSHA Saini: *George*

Wadhifa: MSIMAMIZI WA MRANI Tarehe: 11-03-2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ABRAHAM MBUGHUNI Saini: *Abraham*

Wadhifa: MWENYECUJI KAMATI  
YA UTEKELEZAJI Tarehe: 11/3/2022

